# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHTASARI WA

# KISWAHILI

## KWA SKULI ZA MSINGI

## DARASA LA I – VI

**© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali 2009**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigisha chapa au kutoa muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

**Umetayarishwa na:**

**IDARA YA MITAALA NA MITIHANI**

**S.L.P. 3070**

**ZANZIBAR**

**YALIYOMO**

Ukurasa

**UTANGULIZI** ..... v
Sababu za kuandika Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi ..... v
Umuhimu wa Somo la Kiswahili ..... vi
Madhumuni ya Elimu Zanzibar ..... viii
Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi ..... viii
Ujuzi wa Jumla wa Somo la Kiswahili ..... ix
Malengo ya Jumla ya Somo la Kiswahili ..... x
Uchaguzi na Mpangilio wa Mada ..... xi
Muundo wa Muhtasari ..... xii
**DARASA LA KWANZA** ..... 1
UJUZI ..... 1
MALENGO ..... 2
**DARASA LA PILI** ..... 16
UJUZI ..... 16
MALENGO ..... 17
**DARASA LA TATU** ..... 33
UJUZI ..... 33

MALENGO....................................................................................................34
**DARASA LA NNE**....................................................................................................51
UJUZI....................................................................................................51
MALENGO....................................................................................................52
**DARASA LA TANO**....................................................................................................69
UJUZI....................................................................................................69
MALENGO....................................................................................................70
**DARASA LA SITA**....................................................................................................86
UJUZI....................................................................................................86
MALENGO....................................................................................................87

**UTANGULIZI**

Huu ni muhtasari mpya wa somo la Kiswahili litakalofundishwa kwa madarasa ya I – VI.Somo hili lina umuhimu wa pekee katika mtaala kwa sababu Kiswahili ni lugha ya Taifa na kinatumiwa na Wanzanzibari wote. Katika utangulizi huu unatolewa ufafanuzi wa sababu za kuandika mtaala mpya na umuhimu wa somo lenyewe. Kisha zinatolewa orodha za Madhumuni ya Elimu Zanzibar na ya Elimu ya Msingi; Ujuzi unaotarajiwa kuoneshwa na walengwa na Malengo ya kufundisha somo hili. Mwisho kuna maelezo ya uchaguzi na mpangilio wa mada na ya muundo wa muhtasri na vipengele vyake.

**Sababu za Kuandika Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi.**

Mnamo mwaka 2008/2009 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliendesha mchakato wa kufanya mapitio, kufupisha na kuandika upya mtaala wa elimu ya msingi. Madhumuni yalikuwa ni kufanya mtaala ushabihiane na Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006). Sera hii inalenga kurekebisha ubora na muundo wa elimu ya msingi; kuweka muunganiko bayana kati ya elimu ya maandalizi,msingi na sekondari ili kukidhi matarajio ya walengwa na jamii yao. Sera ya Elimu ya 2006 imebadili muundo wa elimu kwa kutamka kuwa elimu ya maandalizi itakuwa ni sehemu ya elimu ya lazima, elimu ya msingi itakuwa ni ya miaka sita badala ya saba na baadhi ya masomo ya ngazi ya msingi yatafundishwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza kwa madarasa ya Tano na Sita.

Mambo mengine yaliyochochea mapitio haya ni pamoja na yafuatayo:

- Mwelekeo wa kiulimwengu katika maendeleo ya kijamii, kisayansi na kiteknolojia.
- Mwitiko wa serikali kwa Wazanzibari kudai nafasi zaidi za skuli kwa watoto wote na kuongeza ubora wa elimu inayotolewa.
- Mwitiko wa serikali kwa matokeo ya Utafiti wa Mahitaji katika Mtaala wa Elimu ya Msingi wa 2008.

Utafiti wa Mahitaji katika mtaala wa Elimu ya Msingi (2008) ulizingatia mapungufu yafuatayo ya mtaala wa 1998:

- Haukukuza stadi za kuwasiliana, ubunifu na fikra yakinifu.
- Haukuzingatia vya kutosha mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na masuala mtambuka.
- Ulihimiza matumizi ya mbinu za kufundishia/kujifunzia zilizojikita kwa mwalimu zaidi kuliko kwa mwanafunzi.
- Ufundishaji/ujifunzaji ulikuwa wa kinadharia zaidi kuliko kuwa wa vitendo au ushiriki wa wanafunzi.

Kutokana na changamoto kama hizo serikali ilifanya maamuzi kadhaa ya msingi. Miongoni mwa hayo ni kuelekeza kuwa elimu ya msingi iwe miaka sita (6) badala ya saba (7). Vile vile, ilielekeza kwamba mtaala utilie mkazo ukuzaji wa stadi, maarifa na mwenendo bora wa wanafunzi badala ya kuwakaririsha maarifa tu. Moja ya stadi hizo ni kuwasiliana katika lugha mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kiswahili. Iliamuliwa pia kwamba uwekwe muunganiko bayana kati ya mitaala ya maandalizi, msingi na sekondari ili kuepuka kurudia rudia mada.

**Umuhimu wa Somo la Kiswahili**

Kiswahili, kama lugha nyingine, ni njia muhimu sana katika mawasiliano. Lugha ni kibebeo cha ustaarabu na utamaduni wa jamii. Nchini Zanzibar, Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa na huzungumzwa na Wazanzibari wote. Vile vile, Kiswahili ndiyo lugha kuu ya kuendeshea shughuli za serikali ikifuatiwa na Kiingereza.

Katika elimu, Kiswahili ni lugha ya kufundishia katika ngazi za madarasa ya elimu ya maandalizi na elimu ya msingi. Kadhalika, Kiswahili ni lugha ya kuendeshea biashara na hivyo kukuza uchumi wa watu binafsi na serikali. Zaidi ya hayo, lugha hii ni kioo cha utamaduni wa Zanzibar na kichocheo cha uzalendo na umoja wa nchi. Aidha, Kiswahili huwaunganisha Wazanzibari na jamii za jirani na hivyo kustawisha uhusiano mwema wa Tanzania, Afrika Mashariki na mataifa mengine ulimwenguni.

Muhtasari huu utatumiwa na walimu na wanafunzi katika skuli za msingi. Unachukua nafasi ya Muhtasari wa Kiswahili uliotolewa na serikali mwaka 1998. Toleo hili linazingatia stadi zote nne za lugha, kama ifuatavyo:

***Kusikiliza na kuongea***

Hizi ni stadi muhimu kwa mwanafunzi zinazoimarisha usikivu na uelewa wa mambo mbalimbali. Humwezesha mwanafunzi kumudu matamshi sahihi ya maneno ya Kiswahili. Aidha, humpa mwanafunzi uwezo wa kujieleza kwa kujiamini. Kwa hivyo zinapaswa kufundishwa/kufunzwa vyema.

***Kusoma***

Kusoma ni stadi muhimu kwa mwanafunzi kwa vile humtayarisha kuelewa na kutafsiri mambo anayoyasoma. Usomaji hufanyika kwa sauti au kimya kimya. Wakati tunapofundisha wanafunzi kusoma mkazo utiliwe katika matamshi bora, viimbo, shada na mahadhi.

Mwanafunzi akijua kusoma hukielewa kile akisomacho. Vile vile huweza kujieleza akaeleweka vyema. Mwanafunzi mwenye stadi hizo ataweza kutumia muda wa ziada kujisomea na hivyo atapanua msamiati wake, atajitafutia maarifa toka vyanzo anuai na atajenga tabia ya kupenda kujisomea.

***Kuandika***

Kuandika ni stadi muhimu ya mawasiliano na uwekaji wa kumbukumbu za aina mbalimbali. Katika ulimwengu wa sasa mtu asiyeweza kuandika anakabiliwa na vikwazo vya kimawasiliano. Kwa hiyo, inabidi kila mwanafunzi awezeshwe kupata na kutumia stadi hii.

**Madhumuni ya Elimu Zanzibar**

Madhumuni ya elimu Zanzibar ni :

1. Kukuza na kudumisha tabia na desturi bora za Wazanzibari na Watanzania ili kuimarisha umoja na utambulisho wao wa kiutamaduni.
2. Kuimarisha upatikanaji na matumizi sahihi ya aina mbalimbali za maarifa, stadi na mwelekeo/mwenendo kwa ajili ya kuendeleza kikamilifu utu na ubora wa maisha ya jamii.
3. Kuwezesha kila mwananchi kuelewa na kuheshimu misingi ya Katiba ya Zanzibar na ya Tanzania, Haki za Binadamu, pamoja na haki, wajibu na majukumu ya kiraia.
4. Kuendeleza na kuhimiza matumizi bora, uangalizi na utunzaji wa mazingira.
5. Kukuza utashi na heshima ya kufanya kazi za kujiajiri na kuajiriwa pamoja na nidhamu kazini na utendaji kazi kwa kiwango cha juu cha ubora.
6. Kukuza na kudumisha misingi ya kuvumiliana, amani, upendo, haki, maelewano, haki za binadamu na uhuru, umoja wa kitaifa na kimataifa kama vinavyofafanuliwa katika mikataba ya kimataifa.

**Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi**

Madhumuni na malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar ni :

1. Kuwezesha watoto wote wenye umri wa kwenda skuli kujenga na kudumisha misingi imara ya stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, ubunifu na mawasiliano kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyengine za kigeni.
2. Kuwezesha wanafunzi kuelewa matumizi ya sayansi na teknolojia na kutambua mchango wake katika maendeleo ya taifa lao na ulimwengu.

3. Kuweka, kuendeleza na kudumisha miongoni mwa wanafunzi misingi imara ya stadi za kufikiri na udadisi ili kuelewa mazingira yao na mahusiano ya kijamii.
4. Kuwezesha wanafunzi kuelewa jinsi matukio yaliyopita yanavyoathiri matukio ya wakati uliopo na ya wakati ujao.
5. Kugundua vipaji vya kila mwanafunzi kuanzia umri mdogo ili kuvidumisha na kuviendeleza.
6. Kuweka misingi imara ya stadi za uchunguzi fikra na ushirikiano katika kutatua matatizo yanayodumaza maendeleo binafsi ya wanafunzi na ya jamii yao.
7. Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na elimu ya sekondari.
8. Kuwezesha wanafunzi kukuza uwezo wao kiakili na utashi wa kujitafutia maarifa.
9. Kuwazoesha wanafunzi shughuli za uzalishaji mali na kukuza ari yao katika kutekeleza majukumu ya kijamii.
10. Kuwezesha wanafunzi kutambua na kuenzi umoja wa taifa lao pamoja na ushirikiano baina ya taifa lao na watu na mataifa mengine.
11. Kuwezesha wanafunzi kujenga maadili mema kiroho, kiutamaduni na kiitikadi ili kukuza uzalendo na ufahamu wa hali ya nchi yao kihistoria, kisiasa na kijamii.
12. Kukuza na kudumisha nidhamu binafsi ya wanafunzi, kuheshimu usawa na kijinsia na kulinda afya zao na za watu wengine.
13. Kuwezesha wanafunzi kujenga tabia za umaridadi na unadhifu pamoja na matumizi bora ya muda wao wa mapumziko.
14. Kukuza upendo wa wanafunzi kwa mazingira wanayoishi pamoja na utashi wa kuyatunza.

**Ujuzi wa Jumla katika Somo**

Mtaala huu umejikita katika kumpatia ujuzi mwanafunzi (badala ya kujikita katika kufundisha maudhui tu). Ujuzi ni muunganiko sawia wa maarifa, stadi na mwenendo/mwelekeo anavyotarajiwa kuvipata mwanafunzi. Kwa hivyo, baada ya kusoma somo la Kiswahili hadi Darasa la VI wanafunzi wataonesha ujuzi wa:

1. Kuwasiliana kwa usahihi na kujiamini kwa kuzungumza na kuandika katika lugha ya Kiswahili.
2. Kusoma kwa utambuzi na kufupisha matini kwa kuzingatia maana halisi.
3. Kutumia stadi za kupata maarifa ya lugha ya Kiswahili kutoka maktaba na vifaa vingine vya TEHAMA.
4. Kutunga na kuandika kwa usahihi matini mbali mbali kulingana na muktadha.
5. Kusikiliza maelezo na maelekezo toka vyanzo mbali mbali na kuyafuata vilivyo.
6. Kubuni na kuandika kazi mbali mbali za fasihi simulizi na fasihi andishi katika Kiswahili kwa kuzingatia lugha ya kisanii.
7. Kutambua na kutumia vipengele muhimu vya sarufi ya Kiswahili sanifu.
8. Kuhesabu, kuandika na kutumia nambari kwa usahihi katika Kiswahili.
9. Kutafsiri Kiswahili katika lugha za kigeni.

**Malengo ya Jumla ya Somo**

Somo la Kiswahili linafundishwa katika skuli za msingi ili kuwawezesha wanafunzi:

1. Kuwa na tabia ya usomaji katika maktaba na utumiaji wa vifaa vya TEHAMA kwa kujipatia maarifa mapya na burudani.
2. Kufahamu mbinu za mawasiliano katika muktadha na nyakati tofauti.
3. Kupata stadi za usikilizaji, uzungumzaji, usomaji na uandishi sahihi katika Kiswahili.
4. Kuelewa utungaji, ubunifu na uandishi wa kazi mbali mbali za fasihi ya Kiswahili kwa kuzingatia lugha ya kisanii.
5. Kuelewa uchambuzi wa vipengele tofauti vya sarufi ya Kiswahili sanifu.
6. Kufahamu matumizi ya misingi ya tafsiri ya Kiswahili katika lugha nyingine.
7. Kuelewa uhusiano kati ya maneno na nambari katika lugha ya Kiswahili.
8. Kuthamini, kufurahia na kujivunia Kiswahili kama lugha ya Taifa na Kimataifa

**Uchaguzi na Mpangilio wa Mada.**

Katika muhtasari huu mada zimechaguliwa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Mahitaji ya mawasiliano ya kila siku yanayojikita katika stadi kuu nne za lugha, ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.
- Ujenzi wa uhusiano mzuri baina ya watu mbalimbali.
- Uwekaji kumbukumbu za mambo muhimu.
- Ujenzi wa stadi za kifasihi na kisarufi.
- Baadhi ya mada zinajirudia rudia katika madarasa ya juu ili kuimarisha ujuzi na uwezo wa wanafunzi.

Zifuatazo ndizo mada kuu zilizochaguliwa na kusambazwa katika Darasa la I hadi VI.

| NO | MADA KUU | DARASA I | DARASA II | DARASA III | DARASA IV | DARASA V | DARASAVI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kusoma kwa Mazoezi | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 2. | Kusoma kwa Ufahamu. | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 3. | Stadi za Kunukuu | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 4. | Stadi za Utungaji | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 5. | Stadi za Kutafsiri | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 6. | Kusikiliza kwa Ufahamu | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 7. | Mawasiliano | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 8. | Fasihi Simulizi | √ | √ | √ | √ | √ | √ |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 9. | Fasihi Andishi | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 10. | Vipengele vya Sarufi | √ | √ | √ | √ | √ | √ |
| 11. | Kuhesabu, kuandika na kuhusisha Maneno na Nambari. | √ | √ | √ | √ | √ | √ |

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari huu una sehemu kuu mbili: kurasa za mwanzo na jadweli za ufundishaji na ujifunzaji.

**Kurasa za mwanzo**

Sehemu hii inajumuisha jalada la muhtasari, ukurasa wa jina, ukurasa wa mmiliki wa muhtasari na wa yaliyomo. Vile vile, kuna maelezo ya sababu za kuandika mtaala mpya na maelezo ya umuhimu wa somo la Kiswahili. Haya yanafuatiwa na madhumuni ya elimu Zanzibar; malengo ya elimu ya msingi Zanzibar, ujuzi katika somo la Kiswahili na malengo ya somo la Kiswahili. Mwisho, kuna maelezo ya uchaguzi wa mada, pamoja na maelezo ya jadweli ya ufundishaji za ujifunzaji.

**Jadweli za ufundishaji na ujifunzaji**

Sehemu hii inaonesha utaratibu wa ufundishaji na ujifunzaji na imegawika katika madarasa sita. Muhtasari wa kila darasa umetanguliwa na ujuzi ambao wanafunzi wanatakiwa kuonesha katika darasa husika. Kisha kuna malengo yanayotazamiwa kufikiwa katika darasa hilo. Baada ya malengo linafuata jadweli la ufundishaji/ujifunzaji lenye safu wima zenye vichwa vya: Mada Kuu/Mada Ndogo; Malengo Mahsusi; Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia; Vifaa/Zana; Upimaji na Vipindi kwa kila mada ndogo.

***Mada Kuu /Mada Ndogo***

Mada hutamka maudhui yatakayofundishwa. Chini ya mada kuna mada ndogo ambazo huonesha kina na mawanda ya ufundishaji/ujifunzaji wa mada husika.

***Malengo Mahsusi***

Kila mada ndogo imeandikiwa lengo au malengo mahsusi. Hayo yanaeleza stadi, mwenendo/mwelekeo na maarifa ambayo kila mwanafunzi anapaswa kujifunza katika mada ndogo husika. Malengo mahsusi ndiyo yanatumiwa kufanyia upimaji. Aidha, ufikiaji wa malengo mahsusi katika kujifunza hutafsiriwa kama ufikiaji wa stadi, mwelekeo na maarifa yanayolengwa katika mada husika. Kila mwanafunzi darasani anatakiwa kuyafikia malengo mahsusi yaliyotajwa . Hivyo, mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa lugha ya alama inatumiwa kufundisha mwanafunzi kiziwi, na mashine ya Braille au zana mguso zinatumiwa kwa mwanafunzi asiyeona. Kwa makundi mengine yenye mahitaji maalum, mwalimu atumie miongozo, kanuni, zana na mbinu stahiki ipasavyo ili nao wafundishwe/wajifunze barabara.

***Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia***

Safu hii inaonesha baadhi ya mbinu zinazofaa kufundishia/kujifunzia. Ni mbinu shirikishi tu zinazopendekezwa kwa sababu zinahimiza wanafunzi kujitafutia maarifa na kujenga maana kwa kile wanachojifunza. Mbinu hizo ni kama vile majadiliano ya vikundi; maigizo; nyimbo, changanyakete; bungua bongo; ziara za kielimu na kumwalika mgeni.

Mbinu zilizomo katika safu hii ni mapendekezo tu. Mwalimu anashauriwa atumie mbinu nyengine anazozimudu zitakazoshirikisha wanafunzi na kufanikisha ufundishaji/ujifunzaji kulingana na mazingira, mada na umri wa wanafunzi.

***Vifaa/Zana***

Safu hii imesheheni mapendekezo ya zana na vifaa ambavyo vinafaa kutumiwa katika kufundisha/kujifunza kila mada. Mwalimu anashauriwa kuzitumia hizi pamoja na nyengine atakazoona zinafaa au zinapatikana katika mazingira yake.Mwalimu anashauriwa kubuni na kutengeneza zana/vifaa kulingana na upatikanaji wa malighafi katika mazingira yake. Aidha, wanafunzi wahimizwe kufaragua, kubuni na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia kwa kutumia malighafi za bei nafuu zinazopatikana katika mazingira yao.

***Upimaji***

Safu hii inaonesha maelekezo ya upimaji wa wanafunzi. Inampasa mwalimu kupima maendeleo ya kila siku ya wanafunzi wake. Hii itamwezesha kujua uwezo na matatizo ya wanafunzi, ubora wa mbinu za kufundishia/kujifunzia anazozitumia na ubora wa zana/vifaa anavyotumia. Vile vile, upimaji utamwezesha mwalimu kupanga na kutekeleza mikakati ya kuwasaidia wanafunzi wazito. Aidha, upimaji humwezesha mwalimu kupendekeza marekebisho ya mtaala na vitabu vya kufundishia/kujifunzia. Upimaji wa mwisho wa muhula au mwaka huonesha kiwango cha ujuzi alichofikia mwanafunzi.

Kwa sababu hizo, mwalimu anashauriwa kupima maendeleo ya mwanafunzi kila siku, kila mwezi, kila muhula na kila mwaka. Akifanya hivyo, hana budi kuzingatia malengo mahsusi ya kila mada iliyofundishwa na njia mwafaka za upimaji.

**Vipindi**

Safu hii inaonesha makadirio ya idadi ya vipindi vya kufundisha/kujifunza kila mada. Idadi hiyo inafikiwa baada ya kujumlisha idadi ya vipindi kwa mwaka wa masomo (siku 224), kisha kuvigawa kwa idadi ya mada ndogo zilizomo kwenye muhtasari. Vipindi 16 vimepunguzwa Darasa la I, II, III na IV kwa ajili ya mitihani. Katika Darasa la V na VI vipindi 12 vimepunguzwa kwa ajili hiyo pia. Makadirio haya ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Somo la Kiswahili limepangiwa vipindi vinane (8) kwa wiki kwa madarasa ya I – IV na vipindi sita (6) kwa wiki kwa madarasa ya V – VI. Muda wa kipindi kimoja kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi, shifti ya asubuhi, utakuwa dakika 40; utakuwa dakika 35 shifti ya mchana. Siku za Ijumaa muda wa kila kipindi utakuwa dakika 30 tu. Utawala wa skuli unahimizwa kufidia muda wa masomo utakaopotea kutokana na dharura za sikukuu za kidini na za kiserikali.

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

**ZANZIBAR**

# DARASA LA KWANZA

## UJUZI

Baada ya kusoma somo la Kiswahili katika Darasa la I, wanafunzi wataonesha ujuzi wa:-

1. Kusikiliza na kufuata maelekezo kwa usahihi.
2. Kusoma na kuandika maneno na sentensi fupi.
3. Kueleza mahitaji yao kwa kutumia sentensi za msingi za Kiswahili.
4. Kupenda kueleza hadithi fupi fupi, methali na vitendawili katika Kiswahili.
5. Kutumia maktaba na vifaa vingine vya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ili kupata taarifa, kuwasiliana na kujiburudisha.
6. Kubuni, kueleza na kuandika kazi mbali mbali za fasihi simulizi.
7. Kutambua na kutumia vipengele tofauti vya sarufi ya Kiswahili Sanifu.
8. Kutunga na kuandika kazi mbali mbali kwa lugha sanifu kwa ustadi.
9. Kutafsiri maneno ya Kiswahili katika Kiingereza kwa usahihi.
10. Kuhesabu, kuandika na kuhusisha maneno na nambari hadi 2000 kwa usahihi.

**MALENGO**

Malengo ya kufundisha somo la Kiswahili katika Darasa la I ni kuwawezesha wanafunzi:

1. Kufahamu matumizi ya Kiswahili katika kujifunza masomo mbali mbali.
2. Kupata stadi za usomaji na uandishi wa maneno na sentensi fupi fupi kwa usahihi.
3. Kuwa wepesi wa kusikiliza na kufuata maelekezo kwa usahihi.
4. Kuelewa misingi ya ubunifu na tafsiri ya kazi mbali mbali za fasihi simulizi na fasihi andishi.
5. Kufahamu utoaji wa maelezo ya matukio kwa kuzingatia nyakati tofauti.
6. Kupata stadi za matumizi ya maktaba na vifaa vingine vya TEHAMA kwa kupata elimu na burudani.
7. Kutambua matumizi ya vipengele tofauti vya sarufi ya Kiswahili Sanifu.
8. Kupata stadi za utumiaji wa misingi ya uandishi wa kazi mbali mbali kwa lugha sanifu ya Kiswahili.
9. Kufahamu tafsiri ya maneno ya Kiswahili katika Kiingereza.
10. Kujenga stadi za hesabu, uandishi na matumizi ya nambari hadi 2,000 kwa usahihi.

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. KUSOMA KWA MAZOEZI<br>a) Kusoma Maneno kwa Sauti. | Mwanafunzi aweze kutamka kwa usahihi maneno ya lugha ya Kiswahili. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka kwa usahihi maneno ya Kiswahili.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe, mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka kwa usahihi maneno ya lugha ya Kiswahili. | 1. Kadi za picha.<br>2. Kadi za maneno.<br>3. Vitu halisi.<br>4. Kadi katika maandishi ya Braille.<br>5. Chati ya matumizi ya vituo na alama za uandishi.<br>6. Chati mguso.<br>7. Kadi za maneno mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutamka maneno ya lugha ya Kiswahili kwa usahihi? | 14 |
| b) Kusoma Sentensi Fupi Fupi. | Mwanafunzi aweze kusoma sentensi fupi fupi za lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma sentensi fupi fupi kwa usahihi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe, mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma sentensi fupi kwa usahihi. | 1. Kadi za sentensi fupi fupi.<br>2. Kadi za sentensi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma sentensi fupi fupi za lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 14 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Kusoma Majina ya Njia. | Mwanafunzi aweze kutamka kwa usahihi majina ya njia. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka kwa usahihi majina ya njia.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka kwa usahihi majina ya njia. | 1. Kadi za majina ya njia.<br>2. Kadi za maneno za Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutamka majina ya njia kwa usahihi? | 7 |
| d) Kusoma Majina ya Vyakula vya Asili vya Mswahili. | Mwanafunzi aweze kutamka majina ya vyakula vya asili vya Mswahili. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka kwa usahihi majina ya vyakula vya asili vya Mswahili.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka kwa usahihi majina ya vyakula vya asili vya Mswahili. | 1. Kadi za majina ya vyakula vya asili vya Mswahili.<br>2. Kadi za maandishi ya Braille za majina ya vyakula asili vya Mswahili. | Je, mwanafunzi anaweza kutamka majina ya vyakula vya asili ya Mswahili kwa usahihi? | 7 |

| MADA KUU / MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. KUSOMA KWA UFAHAMU<br>Kusoma Sentensi Fupi. | Mwanafunzi aweze kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika sentensi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika sentensi. | 1. Chati ya sentensi mbalimbali.<br>2. Chati mguso.<br>3. Kamusi. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika sentensi? | 14 |
| 3. STADI ZA KUNUKUU.<br>a) Hati za Maneno. | Mwanafunzi aweze kuandika kwa usahihi maneno yaliyojengwa kwa silabi tatu zilizotofautiana. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kwa usahihi maneno yenye silabi tatu tofauti. | 1. Kadi za maneno.<br>2. Kadi za maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika kwa usahihi maneno yaliyojengwa kwa silabi tatu zilizotofautiana? | 12 |
| b) Hati za Sentensi Fupi Fupi. | Mwanafunzi aweze kuandika sentensi fupi fupi kwa mpangilio sahihi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika sentensi fupi fupi kwa mpangilio sahihi. | 1. Vifaa vya kuandikia.<br>2. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika sentensi fupi fupi kwa mpangilio sahihi? | 12 |

| MADA KUU /MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 4. STADI ZA UTUNGAJI. Sentensi za Picha. | Mwanafunzi aweze kutunga sentensi mbali mbali zinazohusiana na picha. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kulinganisha na picha. | 1. Kadi za picha.<br>2. Kadi za sentensi.<br>3. Kadi za picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutunga sentensi mbali mbali zinazohusiana na picha? | 14 |
| 5. STADI ZA KUTAFSIRI<br>a) Kutafsiri Maneno Mafupi kwa Kiingereza. | Mwanafunzi aweze kutoa tafsiri sahihi ya maneno mafupi ya Kiswahili kwa Kiingereza. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutafsiri kwa usahihi maneno mafupi ya Kiswahili kwa Kiingereza. | 1. Kadi za maneno.<br>2. Kadi za maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa tafsiri sahihi ya maneno mafupi ya Kiswahili kwa Kiingereza? | 12 |
| b) Kutafsiri Maneno Marefu kwa Kiingereza. | Mwanafunzi aweze kutoa tafsiri sahihi ya maneno marefu ya Kiswahili kwa Kiingereza. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu awaongoze wanafunzi kutafsiri kwa usahihi maneno marefu ya Kiswahili kwa Kiingereza. | 1.Orodha ya maneno.<br>2. Kadi za maneno katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa tafsiri sahihi ya maneno marefu ya Kiswahili kwa Kiingereza? | 12 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 6. KUSIKILIZA KWA UFAHAMU<br>a) Kusikiliza Habari Fupi. | Mwanafunzi aweze kujibu maswali kutokana na habari aliyoisikiliza. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali kwa usahihi kutokana na habari waliyoisikiliza. | 1. Orodha ya maswali.<br>2. Redio.<br>3. Kanda za kurekodia sauti. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali kutokana na habari aliyoisikiliza? | 14 |
| b) Hadithi Fupi Fupi. | Mwanafunzi aweze kujibu maswali kutokana na hadithi aliyoisikiliza. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali kwa usahihi kutokana na hadithi waliyoisikiliza.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Kisa Mafunzo mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali yanayotokana na hadithi. | 1. Orodha ya maswali.<br>2. Orodha ya maswali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali kutokana na hadithi aliyoisikiliza? | 14 |
| 7. MAWASILIANO<br>a) Kuomba Ruhusa. | Mwanafunzi aweze kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa maombi ya ruhusa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze lugha inayofaa katika muktadha wa maombi ya ruhusa.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo – dhima mwalimu awaongoze wanafunzi namna ya kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa maombi ya ruhusa. | 1. Vifaa vya uigizaji.<br>2. Chati ya msamiati wa kuomba ruhusa.<br>3. Chati mguso.<br>4. Kanda za video. | Je, mwanafunzi anaweza kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa maombi ya ruhusa? | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Kuomba Msamaha. | Mwanafunzi aweze kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa maombi ya msamaha. | 1. Kwa kutumia mhadhara mfupi mwalimu aeleze lugha inayofaa katika muktadha wa maombi ya msamaha.<br>2. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa maombi ya msamaha. | 1. Chati ya msamiati ya kuomba msamaha.<br>2. Chati ya maandishi ya Braille.<br>3. Kanda za video. | Je, mwanafunzi anaweza kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa maombi ya msamaha? | 13 |
| c) Kukubali au Kukataa kwa Heshima. | Mwanafunzi aweze kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa kukubali au kukataa kwa heshima. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa kukubali au kukataa kwa heshima.<br>2. Kwa kutumia igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa kukubali au kukataa kwa heshima. | 1.Vitu mbali mbali.<br>2. Chati ya msamiati wa kukubali au kukataa kwa heshima.<br>3. Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutumia lugha inayofaa katika muktadha wa kukubali au kukataa kwa heshima? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| d) Kutoa Maelezo Shaksia na ya Rafiki zake. | Mwanafunzi aweze kutoa maelezo yake binafsi na ya rafiki zake. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maelezo yao binafsi na ya rafiki zao. | 1. Picha za kujitambulisha na kutambulisha wengine.<br>2. Picha mguso.<br>3. Kanda za kurekodia sauti. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maelezo yake binafsi na ya rafiki zake? | 13 |
| e) Kutoa Maelezo ya Familia. | Mwanafunzi aweze kueleza kuhusu familia yake. | Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi wa mchoro elekezi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza kuhusu familia zao. | 1. Picha za familia.<br>2. Chati ya mti unaoonesha familia.<br>3. Picha na Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza kuhusu familia yake? | 13 |
| f) Kutekeleza Maelekezo Anayopewa. | Mwanafunzi aweze kufuata kwa usahihi maelekezo anayopewa. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kufuata kwa usahihi maelekezo wanayopewa. | 1. Vitu mbali mbali.<br>2. Vifaa vya uigizaji. | Je, mwanafunzi anaweza kufuata kwa usahihi maelekezo anayopewa? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. FASIHI SIMULIZI.<br>a) Nyimbo. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubainisha nyimbo mbali mbali zilizomo katika mazingira yake. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha nyimbo mbali mbali zilizomo katika mazingira yao. | 1. Sampuli za nyimbo.<br>2. Sampuli za nyimbo katika maandishi ya Braille.<br>3. Kanda z kurekodia sauti.<br>4. Kanda za video.<br>5. CDs \ DVD. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha nyimbo mbali mbali zilizomo katika mazingira yake? | 14 |
| | (ii) Kuimba nyimbo mbali mbali. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba nyimbo mbali mbali. | 1. Kanda za redio.<br>2. CDs \ DVD<br>3. Kanda za video. | Je, mwanafunzi anaweza kuimba nyimbo mbali mbali? | |
| | (iii) Kueleza mafunzo yanayojitokeza katika nyimbo. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo yanayojitokeza katika nyimbo. | 1. Nyimbo teule katika maandishi.<br>2. Nyimbo teule katika maandishi ya Braille.. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafunzo yanayojitokeza katika nyimbo? | |
| b) Vitendawili. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutega vitendawili. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutega vitendawili mbali mbali. | 1. Kadi za picha.<br>2. Vitu halisi.<br>3. Vifanani/ modeli<br>4. Kadi za picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutega vitendawili? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kutegua vitendawili kwa usahihi. | Kwa kutumia mbinu ya michezo mwalimu awaongoze wanafunzi kutegua vitendawili mbali mbali kwa usahihi. | 1. Kadi za picha.<br>2. Vitu halisi.<br>3. Vifanani /modeli.<br>4. Kadi za picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutegua vitendawili kwa usahihi? | |
| c) Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutamba hadithi fupi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutamba hadithi fupi. | 1. Chati ya kanuni za utambaji wa hadithi.<br>2. Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutamba hadithi fupi? | 14 |
| | (ii) Kueleza ujumbe unaopatikana katika hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya kisa mafunzo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza ujumbe unaopatikana katika hadithi. | 1. Sampuli ya hadithi katika maandishi.<br>2. Hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza ujumbe unaopatikana katika hadithi? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 9. FASIHI ANDISHI. Kuandika Hadithi Fupi kwa Kutumia Picha. | Mwanafunzi aweze: (i) Kuandika hadithi fupi kutokana na picha. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze namna ya kuandika hadithi fupi kutokana na picha. 2. Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika hadithi fupi kutokana na picha. | 1. Kadi za picha. 2. Kadi za picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika hadithi fupi kutokana na picha? | 14 |
| | (ii) Kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi. | 1. Hadithi katika maandishi. 2. Hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi? | |
| 10. VIPENGELE VYA SARUFI a) Umoja na Wingi. | Mwanafunzi aweze: (i) Kuandika kwa usahihi umoja na wingi wa maneno. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kwa usahihi umoja na wingi wa maneno. | 1. Vitu mbalimbali. 2. Kadi za maneno. 3. Kadi za maneno katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika kwa usahihi umoja na wingi wa maneno? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kubainisha maneno yasiyobadilika katika umoja na wingi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze namna ya kubainisha maneno yasiyobadilika katika umoja na wingi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha maneno yasiyobadilika katika umoja na wingi. | 1. Orodha ya maneno yasiyobadilika katika umoja na wingi.<br>2.Maneno katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha maneno yasiyobadilika katika umoja na wingi? | |
| b) Nyakati za Msingi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutumia nyakati za msingi kwa usahihi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze namna ya kutumia nyakati za msingi kwa usahihi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutumia nyakati za msingi kwa usahihi. | 1. Chati ya nyakati za msingi.<br>2. Chati ya nyakati katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutumia nyakati za msingi kwa usahihi? | 13 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kubainisha nyakati za msingi katika sentensi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha nyakati za msingi katika sentensi. | 1. Chati ya sentensi mbali mbali.<br>2. Kadi za nyakati za msingi.<br>3.Kadi na Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha nyakati za msingi katika sentensi? | |
| c) Kinyume cha Maneno. | Mwanafunzi aweze kutoa kinyume cha maneno mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa kinyume cha maneno mbali mbali. | 1. Vitu halisi.<br>2. Picha za vitu mbali mbali.<br>3. Picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa kinyume cha maneno mbali mbali? | 12 |
| 11. KUHESABU, KUANDIKA NA KUHUSISHA MANENO NA NAMBARI<br>a) Kuhesabu Nambari 1 hadi 2000. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuhesabu kwa usahihi nambari 1 hadi 2000. | Kwa kutumia mbinu burudiko mwalimu awaongoze wanafunzi kuhesabu kwa usahihi nambari 1 hadi 2000. | 1. Kadi za nambari.<br>2. Kadi za nambari mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuhesabu kwa usahihi nambari 1 hadi 2000? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuhusisha maneno na nambari. | Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi mwalimu awaongoze wanafunzi kuhusisha maneno na nambari. | 1. Kadi za maneno.<br>2. Kadi za nambari.<br>3. Kadi za nambari mguso.<br>4. Kadi za maneno mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuhusisha maneno na nambari? | |
| b) Kuandika Nambari 1 hadi 2000. | Mwanafunzi aweze kuandika nambari 1 hadi 2000 kwa usahihi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika nambari 1 hadi 2000 kwa usahihi. | 1. Vifaa vya kuandikia.<br>2. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika nambari 1 hadi 2000 kwa usahihi? | 13 |

## DARASA LA PILI

**UJUZI**

Baada ya kusoma somo la Kiswahili katika Darasa la II, wanafunzi wataonesha ujuzi wa:-

1. Kupenda kusoma kwa utambuzi na kuandika sentensi na habari fupi kwa usahihi.
2. Kusikiliza na kufuata maelekezo kwa usahihi.
3. Kuzungumza juu ya mambo yaliyomo katika mazingira yao kwa kutumia nyakati tatu za msingi.
4. Kupenda kusimulia hadithi fupi fupi, kuelezea methali, kutega na kutegua vitendawili.
5. Kutumia maktaba na vifaa vingine vya TEHAMA ili kupata taarifa, kuwasiliana na kujiburudisha.
6. Kutambua na kutumia vipengele muhimu vya sarufi ya Kiswahili Sanifu.
7. Kutunga na kuandika kazi mbali mbali kwa lugha sanifu kwa ustadi.
8. Kutafsiri sentensi za Kiswahili katika Kiingereza kwa usahihi.
9. Kuhesabu, kuandika na kuhusisha maneno na nambari hadi 5000 kwa usahihi.

**MALENGO**

Malengo ya kufundisha somo la Kiswahili katika Darasa la II ni kuwawezesha wanafunzi:

1. Kuimarisha na kuendeleza stadi za usomaji na uandishi kwa kuzingatia nyakati tatu za msingi.
2. Kuwa wasikivu na wafuatiliaji wa maelekezo kwa usahihi.
3. Kupata stadi za mawasiliano na maelezo ya mahitaji yao kwa ufasaha.
4. Kufahamu utoaji wa maelezo ya matukio kwa kuzingatia nyakati tatu za msingi.
5. Kupata stadi za matumizi ya maktaba na vifaa vya TEHAMA kwa kupata elimu na burudani.
6. Kuelewa misingi ya ubunifu na tafsiri ya kazi mbali mbali za fasihi simulizi na fasihi andishi.
7. Kutambua misingi ya uandishi wa kazi mbali mbali kwa lugha sanifu ya Kiswahili.
8. Kutambua matumizi ya vipengele tofauti vya sarufi ya Kiswahili Sanifu.
9. Kufahamu tafsiri ya sentensi za Kiswahili katika Kiingereza kwa usahihi.
10. Kujenga stadi za hesabu, uandishi na matumizi ya nambari hadi 5,000 kwa usahihi.

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. KUSOMA KWA MAZOEZI.<br>a) Kusoma Sentensi Ndefu. | Mwanafunzi aweze kusoma sentensi ndefu kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma sentensi ndefu kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma sentensi ndefu kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kadi za sentensi.<br>2. Chati za sentensi mbali mbali.<br>3. Kadi za maandishi ya Braille.<br>4. Chati mguso.<br>5. Kanda za kurikodia sauti. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma sentensi ndefu kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 14 |
| b) Kusoma Aya Moja. | Mwanafunzi aweze kusoma aya moja kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma aya moja kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma aya moja kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Chati ya vituo na alama za uandishi.<br>2. Chati mguso.<br>3. Kanda za kurikodia sauti. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma aya moja kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 12 |
| c) Kusoma Habari Fupi. | Mwanafunzi aweze kusoma habari fupi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma habari fupi kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma habari fupi kwa usahihi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Chati ya taratibu za ufupisho.<br>2. Chati mguso.<br>3. Habari katika maandishi<br>4. Habari katika maandishi ya Braille.<br>5. Magazeti. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma habari fupi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 14 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| d) Kusoma na Kuainisha Majina ya Rangi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kusoma kwa usahihi majina ya rangi mbali mbali. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma kwa usahihi majina ya rangi mbalimbali.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma kwa usahihi majina ya rangi mbali mbali. | 1. Kadi za majina ya rangi mbalimbali.<br>2. Kadi za maneno mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma kwa usahihi majina ya rangi mbali mbali? | 13 |
| | (ii) Kubainisha kwa usahihi majina ya rangi mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha kwa usahihi majina ya rangi mbalimbali. | 1. Vitu halisi.<br>2. Vifanani/modeli.<br>3. Vielelezo vya rangi.<br>4. Kadi za majina.<br>5. Kadi za majina mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha kwa usahihi majina ya rangi mbali mbali? | |
| 2. KUSOMA KWA UFAHAMU<br>Kusoma Sentensi Ndefu. | Mwanafunzi aweze kueleza maana ya maneno yaliyotumika katika sentensi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika sentensi. | 1. Kamusi.<br>2. Orodha ya maneno.<br>3. Orodha ya maneno katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya maneno yaliyotumika katika sentensi? | 14 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. STADI ZA KUNUKUU.<br>a) Hati za Sentensi Ndefu. | Mwanafunzi aweze kuandika kwa usahihi sentensi ndefu kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kwa usahihi sentensi ndefu kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kadi za sentensi ndefu.<br>2. Chati za sentensi mbali mbali.<br>3. Maandishi ya Braille.<br>4. Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika kwa usahihi sentensi ndefu kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 12 |
| b) Imla ya Sentensi Fupi Fupi. | Mwanafunzi aweze kuandika imla ya sentensi fupi fupi kwa wepesi na usahihi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze namna ya kuandika imla ya sentensi fupi fupi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya imla mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika sentensi fupi fupi kwa usahihi. | 1. Vitabu vya wanafunzi.<br>2. Vitabu vya wanafunzi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika imla ya sentensi fupi fupi kwa wepesi na usahihi? | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 4. STADI ZA UTUNGAJI<br>Insha ya Picha. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni maelezo mtiririko mnasaba na picha. | Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi mwalimu awaongoze wanafunzi kubuni maelezo mtiririko yanayotokana na picha. | 1. Kadi za picha.<br>2. Kadi za picha mguso.<br>3. Kanda za video.<br>4. CDs.\ DVD | Je, mwanafunzi anaweza kubuni maelezo mtiririko mnasaba na picha? | 14 |
| | (ii) Kujibu maswali yanayohusiana na picha. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali yanayohusiana na picha. | 1. Orodha ya maswali.<br>2. Orodha ya maswali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali yanayohusiana na picha? | |
| 5. STADI ZA KUTAFSIRI<br>a) Kutafsiri Sentensi Fupi Fupi kwa Kiingereza. | Mwanafunzi aweze kutafsiri kwa usahihi sentensi fupi fupi za Kiswahili kwa Kiingereza. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu awaongoze wanafunzi kutafsiri kwa usahihi sentensi fupi fupi za Kiswahili kwa Kiingereza. | 1. Chati ya sentensi.<br>2. Chati ya sentensi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutafsiri kwa usahihi sentensi fupi fupi za Kiswahili kwa Kiingereza? | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Kutafsiri Sentensi Ndefu kwa Kiingereza. | Mwanafunzi aweze kutafsiri kwa usahihi sentensi ndefu za Kiswahili kwa Kiingereza. | Kwa kutumia onesho mbinu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutafsiri kwa usahihi sentensi ndefu za Kiswahili kwa Kiingereza. | 1. Chati ya sentensi ndefu.<br>2. Chati ya sentensi ndefu katika maandishi ya Braille.. | Je, mwanafunzi anaweza kutafsiri kwa usahihi sentensi ndefu za Kiswahili kwa Kiingereza? | 13 |
| 6. KUSIKILIZA KWA UFAHAMU.<br>a) Kusikiliza Habari Fupi. | Mwanafunzi aweze kujibu kwa usahihi maswali kutokana na habari fupi aliyoisikiliza. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu kwa usahihi maswali kutokana na habari waliyoisikiliza. | 1. Orodha ya maswali.<br>2. Orodha ya maswali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu kwa usahihi maswali kutokana na habari fupi aliyoisikiliza? | 14 |
| b) Kusikiliza Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze kujibu kwa usahihi maswali kutokana na hadithi fupi aliyoisikiliza. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu kwa usahihi maswali kutokana na hadithi fupi waliyoisikiliza. | 1. Orodha ya maswali.<br>2.Orodha ya maswali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali kwa usahihi kutokana na hadithi fupi aliyoisikiliza? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 7. MAWASILIANO<br>a) Kueleza Mahitaji Yake ya Msingi. | Mwanafunzi aweze kueleza kwa ufasaha na usahihi mahitaji yake ya msingi katika muktadha mbali mbali. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza kwa ufasaha mahitaji yao katika muktadha mbali mbali. | 1. Chati ya taratibu za kijieleza .<br>2. Chati katika maandishi ya Braille.<br>3. Kanda za video. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza kwa ufasaha na usahihi mahitaji yake katika muktadha mbali mbali? | 12 |
| b) Kutoa Taarifa Fupi za Matukio. | Mwanafunzi aweze kueleza kwa ufupi na ufasaha juu ya matukio mbali mbali yanayotokea katika jamii yake. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa taarifa kwa ufupi juu ya matukio mbali mbali yanayotokea katika jamii yao. | 1. Chati ya matukio muhimu.<br>2. Chati mguso.<br>3. Chati ya taratibu za utoaji wa taarifa.<br>4. Chati ya taratibu za utoaji wa taarifa katika maandishi ya Braille.<br>5. Kanda za video.<br>6., CDs./ DVD | Je, mwanafunzi anaweza kueleza kwa ufupi na ufasaha juu ya matukio mbali mbali yanayotokea katika jamii yake? | 12 |

| **MADA KUU/ MADA NDOGO** | **MALENGO MAHSUSI** | **MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA** | **VIFAA/ZANA** | **UPIMAJI** | **VIPINDI** |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Kutambulisha Familia na Watu Wengine katika Mazingira Yake. | Mwanafunzi aweze kuitambulisha kwa usahihi familia yake na watu wengine. | 1. Kwa kutumia mbinu ya usaili mwalimu awaongoze wanafunzi kuzitambulisha kwa usahihi familia zao na watu wengine.<br>2. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutambulisha kwa usahihi familia zao na watu wengine. | 1. Chati ya mti wa familia.<br>2. Picha za familia.<br>3. Picha na Chati mguso.<br>4. Kanda za video. | Je, mwanafunzi anaweza kuitambulisha kwa usahihi familia yake na watu wengine? | 13 |
| d) Kutoa Maelekezo. | Mwanafunzi aweze kutoa maelekezo kwa usahihi kwa kuzingatia muktadha. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maelekezo kwa usahihi kwa kuzingatia muktadha.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maelekezo kwa usahihi kwa kuzingatia muktadha. | 1. Vifaa vya uigizaji.<br>2. Chati ya utoaji wa maelekezo.<br>3. Chati katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maelekezo kwa usahihi kwa kuzingatia muktadha? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. FASIHI SIMULIZI<br>a) Nyimbo. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutoa mifano ya nyimbo zilizomo katika mazingira yake. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa mifano ya nyimbo zilizomo katika mazingira yao. | 1. Orodha ya nyimbo.<br>2. Orodha ya nyimbo katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa mifano ya nyimbo zilizomo katika mazingira yake? | 14 |
| | (ii) Kuimba nyimbo zilizomo katika mazingira yake. | Kwa kutumia mbinu burudiko mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba nyimbo zilizomo katika mazingira yake. | 1. Kanda za kurekodia sauti.<br>2. Kanda za video. | Je, mwanafunzi anaweza kuimba nyimbo zilizomo katika mazingira yake? | |
| | (iii) Kueleza mafunzo yaliyojitokeza katika nyimbo. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo yaliyojitokeza katika nyimbo. | 1. Sampuli ya nyimbo.<br>2. Sampuli ya nyimbo katika mandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafunzo yaliyojitokeza katika nyimbo? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Vitendawili. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni vitendawili mbali mbali kutokana na mazingira yake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze namna ya kubuni vitendawili kutokana na mazingira.<br>2. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubuni vitendawili kutokana na mazingira. | 1. Orodha ya mifano ya vitendawili.<br>2. Mifano ya vitendawili katika maandishi ya Braille.<br>3. Chati ya taratibu za kubuni vitendawili.<br>4. Chati ya taratibu za kubuni vitendawili katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubuni vitendawili mbali mbali kutokana na mazingira yake? | 14 |
| | (ii) Kutega vitendawili kwa usahihi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutega vitendawili. | 1. Kadi za picha.<br>2. Vitu halisi.<br>3. Vifanani/modeli<br>4. Kadi za picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutega vitendawili kwa usahihi? | |
| | (iii) Kutegua vitendawili vilivyomo katika mazingira yake. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutegua vitendawili vilivyomo katika mazingira yao. | 1. Kadi za picha.<br>2. Vitu halisi.<br>3. Vifanani/modeli<br>4. Kadi za picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutegua vitendawili vilivyomo katika mazingira yake? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni hadithi fupi fupi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze namna ya kubuni hadithi fupi.<br>2. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubuni hadithi kutokana na mazingira yao. | 1. Chati ya vipengele vya ubunifu wa hadithi.<br>2. Chati ya vipengele katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubuni hadithi fupi fupi? | 14 |
| | (ii) Kutamba hadithi fupi. | Kwa kutumia mbinu ya masimulizi mwalimu awaongoze wanafunzi kutambiana hadithi wenyewe kwa wenyewe. | 1. Chati ya taratibu za utambaji wa hadithi.<br>2. Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutamba hadithi fupi? | |
| | (iii) Kueleza ujumbe unaopatikana katika hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza ujumbe unaopatikana katika hadithi. | 1. Hadithi katika maandishi .<br>2. Hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza ujumbe unaopatikana katika hadithi? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 9. FASIHI ANDISHI Kubuni na Kuandika Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze kuandika hadithi fupi za kubuni mwenyewe. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze namna ya kuandika hadithi fupi ya kubuni.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika hadithi fupi ya kubuni. | 1. Vifaa vya kuandikia.<br>2. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika hadithi fupi za kubuni mwenyewe? | 15 |
| 10. VIPENGELE VYA SARUFI<br>a) Nyakati za Msingi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja vipengele vinavyoonesha nyakati za msingi katika maneno au sentensi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vipengele vinavyoonesha nyakati za msingi katika maneno au sentensi. | 1. Kadi za sentensi.<br>2. Kadi za sentensi katika maandishi ya Braille.<br>3. Kadi za silabi za nyakati.<br>4. Kadi za silabi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vipengele vinavyoonesha nyakati za msingi katika maneno au sentensi? | 13 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kubadili sentensi kutoka wakati mmoja kwenda wakati mwingine. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubadili sentensi kutoka wakati mmoja kwenda mwengine. | 1. Orodha ya sentensi yakinishi.<br>2. Sentensi yakinishi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubadili sentensi kutoka wakati mmoja kwenda wakati mwingine? | |
| | (iii) Kutunga sentensi zinazoonesha nyakati mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi zinazoonesha nyakati mbali mbali. | 1. Orodha ya sentensi zinazoonesha nyakati mbali mbali.<br>2. Sentensi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutunga sentensi zinazoonesha nyakati mbali mbali? | |
| b) Ukanushi wa Sentensi Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutunga sentensi katika hali ya ukanushi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi katika hali ya ukanushi. | 1. Orodha ya sentensi za ukanushi.<br>2. Sentensi za ukanushi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutunga sentensi katika hali ya ukanushi? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kubadili sentensi katika hali ya ukanushi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubadili sentensi katika hali ya ukanushi. | 1. Orodha ya sentensi za ukanushi<br>2. Sentensi za ukanushi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubadili sentensi katika hali ya ukanushi? | |
| c) Kinyume cha Maneno. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuorodhesha maneno yenye kinyume. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kuorodhesha maneno yenye kinyume. | 1. Orodha ya maneno yenye kinyume.<br>2. Maneno yenye kinyume katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuorodhesha maneno yenye kinyume? | 13 |
| | (ii) Kutoa kinyume cha maneno mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa kinyume cha maneno mbalimbali. | 1. Orodha ya maneno .<br>2. Orodha ya maneno katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa kinyume cha maneno mbali mbali? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| d) Maneno yenye Maana Sawa. | Mwanafunzi aweze kuorodhesha maneno mbali mbali yenye maana sawa. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuorodhesha maneno mbali mbali yenye maana sawa. | 1. Orodha ya maneno yenye maana sawa.<br>2. Maneno yenye maana sawa katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuorodhesha maneno mbali mbali yenye maana sawa? | 13 |
| 11. KUHESABU, KUANDIKA NA KUHUSISHA MANENO NA NAMBARI<br>a) Kuhesabu Nambari 2001 hadi 5000. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuhesabu kwa usahihi nambari 2001 hadi 5000. | Kwa kutumia mbinu burudiko mwalimu awaongoze wanafunzi kuhesabu kwa usahihi nambari 2001 hadi 5000. | 1. Kadi za nambari.<br>2. Kadi za maneno.<br>3. Kadi za maneno katika maandishi ya Braille.<br>4. Kadi za nambari mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuhesabu kwa usahihi nambari 2001 hadi 5000? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuhusisha maneno na nambari. | Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kuhusisha maneno na nambari. | 1. Kadi za maneno.<br>2. Kadi za maneno mguso.<br>3. Kadi za nambari.<br>4. Kadi za nambari mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuhusisha maneno na nambari? | |
| b) Kuandika Nambari 2001 hadi 5000 | Mwanafunzi aweze kuandika kwa usahihi nambari 2001 hadi 5000. | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kwa usahihi 2001 hadi 5000. | 1. Vifaa vya kuandikia.<br>2. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika kwa usahihi nambari 2001 hadi 5000? | 13 |

## DARASA LA TATU

**UJUZI**

Baada ya kusoma somo la Kiswahili katika Darasa la III, wanafunzi wataonesha ujuzi wa:-

1. Kusoma matini anuai kwa utambuzi na burudani.
2. Kuandika na kuzungumza Kiswahili kwa usahihi ili kukidhi mahitaji ya muktadha mbali mbali.
3. Kueleza shughuli mbali mbali zinazohusiana na mazingira yao.
4. Kutumia maktaba na vifaa vingine vya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawsiliano) kwa usahihi ili kupata taarifa, kuwasiliana na kujiburudisha.
5. Kusikiliza na kufuata maelekezo kwa usahihi.
6. Kubuni, kueleza na kutafsiri kazi mbali mbali za fasihi simulizi na fasihi andishi kwa njia tofauti.
7. Kutambua, kuainisha na kutumia vipengele tofauti vya sarufi ya Kiswahili Sanifu.
8. Kutafsiri kwa usahihi aya fupi za Kiswahili katika Kiingereza.
9. Kuhesabu, kuandika na kuhusisha maneno  na nambari hadi 50,000 kwa usahihi.
10. Kutunga na kuandika kazi mbali mbali kwa lugha sanifu kwa ustadi.

**MALENGO**

Malengo ya kufundisha somo la Kiswahili katika Darasa la III ni kuwawezesha wanafunzi:

1. Kupenda usomaji na usikilizaji wa habari kwa ufahamu na burudani .
2. Kufahamu utoaji wa taarifa za matukio katika mazingira yao kwa kuzingatia nyakati tofauti.
3. Kuelewa misingi ya ubunifu na tafsiri ya kazi mbali mbali za fasihi simulizi na fasihi andishi.
4. Kufahamu misingi ya utunzi na uandishi wa kazi mbali mbali kwa lugha sanifu ya Kiswahili.
5. Kutambua na kutoa ufafanuzi wa vipengele tofauti vya sarufi ya Kiswahili Sanifu.
6. Kupata stadi za matumizi ya maktaba na zana nyingine za TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawsiliano) ili kupata elimu na burudani.
7. Kufahamu tafsiri ya aya fupi fupi za Kiswahili katika Kiingereza.
8. Kuelewa hesabu, uandishi na matumizi ya nambari hadi 50,000 kwa usahihi.

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. KUSOMA KWA MAZOEZI<br>a) Kusoma Habari Ndefu. | Mwanafunzi aweze kusoma habari ndefu kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma habari ndefu kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma habari ndefu kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Maandishi ya Braille.<br>2. Chati ya matumizi ya vituo mbalimbali.<br>3. Chati mguso.<br>4. Kanda za kurekodi sauti. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma habari ndefu kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 14 |
| b) Kusoma Matangazo ya Biashara. | Mwanafunzi aweze kusoma matangazo ya biashara kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma matangazo ya biashara kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe, mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma matangazo ya biashara kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Mabango mbali mbali ya matangazo ya biashara.<br>2. Chati ya vituo na alama za uandishi .<br>3. Chati mguso.<br>4. Kanda za video. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma matangazo ya biashara kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Kusoma Matangazo ya Nafasi za Kazi. | Mwanafunzi aweze kusoma matangazo ya nafasi za kazi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma matangazo ya nafasi za kazi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma matangazo ya nafasi za kazi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Sampuli ya matangazo ya nafasi za kazi katika magazeti.<br>2. Matangazo ya nafasi za kazi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma matangazo ya nafasi za kazi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 13 |
| 2. KUSOMA KWA UFAHAMU<br>a) Kusoma Aya na Habari Fupi. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika aya na habari fupi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika aya na habari fupi. | 1. Kamusi.<br>2. Sampuli ya aya na habari.<br>3. Sampuli ya aya na habari katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika aya na habari fupi? | 16 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kujibu maswali kutokana na aya na habari fupi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali kutokana na aya na habari fupi. | Orodha ya maswali. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali kutokana na aya na habari fupi? | |
| b) Kusoma Hadithi za Picha. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza hadithi inayotokana na picha. | Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza hadithi inayotokana na picha. | 1. Kadi za picha.<br>2. Kadi za picha mguso.<br>3. CDs.\ DVD<br>4. Kanda za video. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza hadithi inayotokana na picha? | 12 |
| | (ii) Kujibu maswali yanayotokana na picha. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali yanayotokana na picha. | Orodha ya maswali. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali yanayotokana na picha? | |

| MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. STADI ZA KUNUKUU.<br>a) Hati za Habari Fupi. | Mwanafunzi aweze<br>(i) Kuandika habari inayosomeka vizuri na kuzingatia taratibu za uandishi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika habari inayosomeka vizuri na kuzingatia taratibu za uandishi. | 1. Vifaa vya kuandikia.<br>2. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika habari inayosomeka vizuri na kuzingatia taratibu za uandishi? | 12 |
| b) Imla ya Habari Fupi. | Mwanafunzi aweze kuandika habari fupi kwa wepesi na usahihi. | Kwa kutumia mbinu ya imla mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika habari fupi kwa wepesi na usahihi. | 1. Chati ya taratibu za uandishi wa imla.<br>2. Chati ya tratibu za uandishi wa imla katika mandsishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika habari fupi kwa wepesi na usahihi? | 12 |
| 4. STADI ZA UTUNGAJI.<br>a) Barua za Kawaida. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja vipengele muhimu vya uandishi wa barua za kawaida. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze vipengele muhimu vya uandishi wa barua za kawaida.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vipengele muhimu vya uandishi wa barua za kawaida. | 1. Chati ya vipengele vya barua za kawaida.<br>2. Sampuli ya barua katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vipengele muhimu vya uandishi wa barua za kawaida? | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuandika barua za kawaida. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika barua za kawaida.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika barua ya kawaida | 1. Sampuli ya barua ya kawaida.<br>2. Sampuli ya barua ya kawaida katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika barua za kawaida? | |
| b) Kadi za Mwaliko. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kutaja vipengele muhimu vya uandishi wa kadi za mwaliko. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze vipengele muhimu vya uandishi wa kadi za mwaliko.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vipengele muhimu vya uandishi wa kadi za mwaliko. | 1. Chati ya vipengele vya kadi za mwaliko.<br>2. Chati ya vipengele vya kadi za mwaliko katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vipengele muhimu vya uandishi wa kadi za mwaliko? | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuandika kadi za mwaliko. | Kwa kutumia onesho – mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kadi za mwaliko. | 1. Sampuli ya kadi ya mwaliko.<br>2.Kadi ya mwaliko<br>3. katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika kadi za mwaliko? | |
| 5. STADI ZA KUTAFSIRI.<br>.Kutafsiri Aya Fupi fupi kwa Kiingereza. | Mwanafunzi aweze kutafsiri kwa usahihi aya fupi fupi za Kiswahili kwa Kiingereza. | 1. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili maana ya jumla inayojitokeza katika aya.<br><br>2. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutafsiri aya fupi fupi za Kiswahili kwa Kiingereza kwa usahihi. | 1. Aya fupi.<br>2. Aya fupi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutafsiri kwa usahihi aya fupi fupi za Kiswahili kwa Kiingereza? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 6. KUSIKILIZA KWA UFAHAMU<br>a) Kusikiliza Habari Ndefu na Maelezo ya Tukio. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kujibu maswali kutokana na habari ndefu aliyoisikiliza. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali kutokana na habari ndefu aliyosikiliza. | 1. Kanda za kurikodi.<br>2. Kanda za video/TV, CD.<br>3. Orodha ya maswali.<br>4. Habari ndefu katika maandishi.<br>5. Habari ndefu katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali kutokana na habari ndefu aliyoisikiliza? | 14 |
| | (ii) Kueleza kwa ufupi matukio mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza kwa ufupi matukio mbali mbali. | 1. Magazeti.<br>2. Chati ya taratibu za uwasilishaji wa matukio.<br>3. Chati ya taratibu za uwasilishaji wa matukio katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza kwa ufupi matukio mbali mbali kwa ufupi? | |
| b) Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze kujibu maswali yanayotokana na hadithi fupi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali yanayotokana na hadithi fupi. | 1. Kanda za kurekodia sauti.<br>2. Kanda za video.<br>3. Hadithi ndogo katika maandishi.<br>4. Hadithi katika maandishi mguso.<br>5. Orodha ya maswali. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali yanayotokana na hadithi fupi? | 14 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 7. MAWASILIANO<br>a) Kutoa Taarifa za Matukio. | Mwanafunzi aweze kutoa maelezo ya matukio mbalimbali. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu atoe maelezo namna ya kutoa taarifa za matukio mbali mbali.<br>2. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maelezo ya matukio mbali mbali. | 1. Chati ya matukio mbali mbali.<br>2. Kanda za video/CDs/DVD.<br>3. Chati ya matukio katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maelezo ya matukio mbali mbali? | 13 |
| b) Kueleza Umuhimu wa Vitu Vilivyo Karibu Naye. | Mwanafunzi aweze kueleza kwa ufasaha umuhimu wa vitu mbali mbali vilivyomo katika mazingira yake. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza kwa ufasaha umuhimu wa vitu mbali mbali vilivyomo katika mazingira yao. | Vitu halisi mbali mbali. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza kwa ufasaha umuhimu wa vitu mbali mbali vilivyomo katika mazingira yake? | 13 |
| c) Kusimulia Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze kusimulia hadithi fupi inayohusisha mazingira yake. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusimulia hadithi fupi inayohusisha mazingira yao. | 1. Hadithi fupi katika maandishi.<br>2. Hadithi fupi katika maandishi ya Braille<br>3. Chati ya taratibu za kusimulia hadithi.<br>4. Chati ya taratibu za kusimulia hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kusimulia hadithi fupi inayohusisha mazingira yake? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. FASIHI SIMULIZI<br>a) Nyimbo | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni nyimbo fupi fupi. | 1. Kwa kutumia mhadhara mfupi mwalimu aeleze namna ya kubuni nyimbo.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi na kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kubuni nyimbo fupi fupi. | 1. Chati ya vipengele vya nyimbo.<br>2. Chati ya vipengele vya nyimbo katika maandishi ya Braille.<br>3. Sampuli ya nyimbo.<br>4. Sampuli ya nyimbo katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubuni nyimbo fupi fupi? | 13 |
| | (ii) Kuimba nyimbo fupi fupi zenye maadili ya Kizanzibari. | Kwa kutumia onesho mbinu, mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba nyimbo fupi fupi zenye maadili ya Kizanzibari. | 1. Kanda za kunasia sauti<br>2. Kanda za video.<br>3. Kinasa sauti. | Je, mwanafunzi anaweza kuimba nyimbo fupi fupi zenye maadili ya Kizanzibari? | |
| | (iii) Kutoa mafunzo yanayopatikana katika nyimbo. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa mafunzo yanayopatikana katika nyimbo. | 1. Nyimbo katika maandishi.<br>2. Nyimbo katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa mafunzo yanayopatikana katika nyimbo? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Vitendawili. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni vitendawili kwa kuhusisha na mazingira. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubuni vitendawili kwa kuhusisha na mazingira. | 1. Chati ya taratibu za kubuni vitendawili.<br>2. Chati ya maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubuni vitendawili kwa kuhusisha na mazingira? | 13 |
| | (ii) Kutegua vitendawili kwa usahihi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu , mwalimu awaongoze wanafunzi kutegua vitendawili kwa usahihi. | 1. Orodha ya vitendawili.<br>2. Vitendawili katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutegua vitendawili kwa usahihi? | |
| | (iii) Kueleza maana inayopatikana katika vitendawili. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana inayopatikana katika vitendawili. | 1. Orodha ya vitendawili.<br>2. Vitendawili katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana inayopatikana katika vitendawili? | |
| c) Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni hadithi fupi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubuni hadithi fupi. | 1. Chati ya taratibu za kubuni hadithi.<br>2.Chati ya maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubuni hadithi fupi? | 15 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kutamba hadithi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutamba hadithi. | 1. Chati ya taratibu za utambaji wa hadithi.<br>2. Chati ya maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutamba hadithi? | |
| | (iii) Kueleza mafunzo ya hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo ya hadithi. | 1. Sampuli ya hadithi katika maandishi.<br>2. Hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafunzo ya hadithi? | |
| d) Methali. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutoa methali. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa methali. | 1. Sampuli ya methali.<br>2. Sampuli ya methali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa methali? | 13 |
| | (ii) Kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali. | 1. Orodha ya methali.<br>2. Orodha ya methali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali? | |

| MADA KUU/<br>MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| e) Ngonjera. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza vipengele vya ngonjera. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze vipengele vya ngonjera. | 1. Chati ya vipengele vya ngonjera.<br>2. Chati ya maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza vipengele vya ngonjera? | 14 |
| | (ii) Kutamba ngonjera. | Kwa kutumia mbinu – burudiko mwalimu awaongoze wanafunzi kutamba ngonjera. | 1. Sampuli ya ngonjera.<br>2. Sampuli ya ngonjera katika maandishi ya Braille.<br>3. TV. | Je, mwanafunzi anaweza kutamba ngonjera? | |
| | (iii) Kueleza ujumbe unaopatikana katika ngonjera. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza ujumbe unaopatikana katika ngonjera. | 1. Ngonjera katika maandishi.<br>2. Ngonjera katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza ujumbe unaopatikana katika ngonjera? | |
| 9. FASIHI ANDISHI<br>Kubuni na Kuandika Hadithi Ndefu. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuandika hadithi ndefu za kubuni mwenyewe. | 1.Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika hadithi ndefu za kubuni. | 1. Vifaa vya kuandikia.<br>2. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika hadithi ndefu za kubuni mwenyewe? | 16 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika hadithi za kubuni | | | |
| | (ii) Kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi ndefu. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi ndefu. | 1. Hadithi ndefu katika maandishi.<br>2. Hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi ndefu? | |
| 10. VIPENGELE VYA SARUFI<br>a) Ukanushi wa Sentensi Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutunga sentensi fupi katika hali ya ukanushi. | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi fupi katika hali ya ukanushi. | 1. Chati ya sentensi kanushi.<br>2. Chati katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutunga sentensi fupi katika hali ya ukanushi? | 13 |
| | (ii) Kubadili sentensi katika hali ya ukanushi. | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kubadili sentensi katika hali ya ukanushi. | 1. Chati ya sentensi mbali mbali.<br>2. Chati katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubadili sentensi katika hali ya ukanushi? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Kinyume cha Maneno. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuorodhesha maneno yenye kinyume. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kuorodhesha maneno yenye kinyume. | 1. Chati ya maneno yenye kinyume.<br>2. Chati ya maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuorodhesha maneno yenye kinyume? | 10 |
| | (ii) Kutoa kinyume cha maneno. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa kinyume cha maneno. | 1. Kadi za maneno yenye kinyume.<br>2. Chati za maneno katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa kinyume cha maneno? | |
| c) Aina za Maneno. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya nomino, viwakilishi na vivumishi. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya nomino, viwakilishi na vivumishi. | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza:<br>1. Kueleza maana ya nomino?<br>2. Kueleza maana ya viwakilishi?<br>3. Kueleza maana ya vivumishi? | 16 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kutaja aina za nomino, viwakilishi na vivumishi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja aina za nomino, viwakilishi na vivumishi. | 1. Chati ya aina za nomino, viwakilishi na vivumishi.<br>2. Chati ya maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza:<br>1. Kutaja aina za nomino?<br>2. Kutaja aina za viwakilishi?<br>3. Kutaja aina za vivumishi? | |
| | (iii) Kutumia nomino, viwakilishi na vivumishi katika sentensi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutumia nomino, viwakilishi na vivumishi katika sentensi.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe, mwalimu awaongoze wanafunzi kutumia namino, viwakilishi na vivumishi katika sentensi. | 1. Orodha ya nomino, viwakilishi na vivumishi.<br>2. Orodha ya nomino, viwakilishi na vivumishi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza:<br>1. Kutumia nomino katika sentensi?<br>2. Kutumia viwakilishi katika sentensi?<br>3. Kutumia vivumishi katika sentensi? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iv) Kubainisha nomino, viwakilishi na vivumishi katika sentensi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha nomino, viwakilishi na vivumishi katika sentensi.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe, mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha nomino, vivumishi na viwakilishi katika sentensi. | 1. Chati ya sentensi zilizobainishwa Nomino, Viwakilishi na Vivumishi.<br>2. Chati ya maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza<br>1. Kubainisha nomino katika sentensi?<br>2. Kubainisha viwakilishi katika sentensi?<br>3. Kubainisha vivumishi katika sentensi? | |
| 11. KUHESABU, KUANDIKA NA KUHUSISHA MANENO NA NAMBARI<br>a) Kuhesabu Nambari 5001 hadi 50,000. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuhesabu kwa usahihi nambari 5001 hadi 50,000. | Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kuhesabu kwa usahihi nambari 5001 hadi 50,000. | 1. Kadi za nambari.<br>2. Kadi za nambari mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuhesabu kwa usahihi nambari 5001 hadi 50,000? | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuhusisha nambari na maneno. | Kwa kutumia mbinu ya michezo mwalimu awaongoze wanafunzi kuhusisha nambari na maneno. | 1. Kadi za maneno.<br>2. Kadi za nambari.<br>3. Kadi za nambari na za maneno katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuhusisha nambari na maneno? | |
| b) Kuandika Nambari 5001 hadi 50,000. | Mwanafunzi aweze kuandika kwa usahihi nambari 5001 hadi 50,000. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kwa usahihi nambari 5001 hadi 50,000. | 1. Vifaa vya kuandikia.<br>2. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika kwa usahihi nambari 5001 hadi 50,000? | 12 |

## DARASA LA NNE

**UJUZI**

Baada ya kusoma somo la Kiswahili katika Darasa la IV, wanafunzi wataonesha ujuzi wa:-

1. Kusikiliza na kufuata maelekezo kwa usahihi.
2. Kusimulia kwa ufasaha hadithi fupi fupi na matukio mingine yanayohusiana na mazingira yao.
3. Kusoma matini anuai kwa utambuzi na burudani.
4. Kubainisha na kutumia vipengele vya sarufi ya Kiswahili Sanifu.
5. Kutumia maktaba na vifaa vingine vya TEHAMA kwa usahihi ili kupata taarifa, kuwasiliana na kujiburudisha.
6. Kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kwa ufasaha katika kufanya na kuitikia maombi mbali mbali.
7. Kubuni, kueleza na kutafsiri kazi mbali mbali za fasihi simulizi na fasihi andishi kwa njia tofauti.
8. Kutambua na kutumia misingi ya utungaji katika kuandika kazi mbali mbali kwa lugha sanifu ya Kiswahili.
9. Kufupisha sentensi na aya fupi fupi kwa kuzingatia maana halisi.
10. Kutafsiri kwa usahihi aya ndefu za Kiswahili katika Kiingereza.
11. Kuhesabu, kuandika na kuhusisha maneno  na nambari hadi 500,000 kwa usahihi.

**MALENGO**

Malengo ya kufundisha somo la Kiswahili katika Darasa la IV ni kuwawezesha wanafunzi:

1. Kufahamu usikilizaji na uandishi wa habari na taarifa fupi fupi za Kiswahili kwa usahihi.
2. Kufahamu utoaji wa taarifa za matukio yanayohusiana na mazingira yao kwa kuzingatia nyakati tofauti.
3. Kupata stadi za matumizi ya maktaba na vifaa vya TEHAMA ili kupata elimu na burudani.
4. Kutambua matumizi ya vipengele mbali mbali vya sarufi ya Kiswahili Sanifu.
5. Kufahamu misingi ya utunzi na uandishi wa kazi mbali mbali kwa lugha sanifu ya Kiswahili.
6. Kuelewa misingi ya ubunifu na tafsiri ya kazi mbali mbali za fasihi simulizi na fasihi andishi.
7. Kufahamu tafsiri ya aya ndefu za Kiswahili katika Kiingereza.
8. Kujenga stadi za hesabu, uandishi na matumizi ya nambari hadi 500,000 kwa usahihi.

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. KUSOMA KWA MAZOEZI<br>a) Kusoma Matini Fupi. | Mwanafunzi aweze kusoma matini fupi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma matini fupi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma matini fupi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Maandishi ya Braille.<br>2. Chati ya matumizi ya vituo mbalimbali.<br>3. Chati ya maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma matini fupi kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 14 |
| b) Kusoma Magazeti Yaliyoandikwa kwa Kiswahili. | Mwanafunzi aweze kusoma magazeti yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma magazeti yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi. | 1. Magazeti mbali mbali ya Kiswahili.<br>2. Magazeti katika maandishi ya Braille.<br>3. Chati ya vituo na alama za uandishi.<br>4. Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kusoma magazeti yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia vituo na alama za uandishi? | 14 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. KUSOMA KWA UFAHAMU<br>a) Kusoma Matini Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika matini fupi | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika matini. | 1. Kamusi.<br>2. Matini katika maandishi.<br>3. Matini katika maandishi ya Braille.<br>4. Kanda za kurikodia sauti. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maana ya maneno yaliyotumika katika matini fupi? | 15 |
| | (ii) Kutunga sentensi kwa kutumia maneno teule. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno teule. | 1. Orodha ya maneno teule.<br>2.Maneno katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutunga sentensi kwa kutumia maneno teule? | |
| | (iii) Kujibu maswali yanayotokana na matini. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali yanayotokana na matini. | 1. Orodha ya maswali.<br>2. Maswali mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali yanayotokana na matini? | |
| b) Kusoma Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kujibu maswali yanayotokana na hadithi fupi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali yanayotokana na hadithi fupi. | 1.Sampuli ya hadithi fupi.<br>2. Sampuli ya hadithi katika maandishi ya Braille.<br>3. Hadithi ya picha.<br>4. Hadithi ya picha mguso.<br>5. Orodha ya maswali.<br>6. Maswali katika maandishi ya Braille | Je, mwanafunzi anaweza kujibu maswali yanayotokana na hadithi fupi? | 15 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kutoa maana ya maneno teule. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maana ya maneno teule. | Kamusi. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maana ya maneno teule? | |
| | (iii) Kueleza hadithi inayotokana na picha. | Kwa kutumia mbinu ya masimulizi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza hadithi inayotokana na picha. | 1. Kadi za picha.<br>2. Kadi za picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza hadithi inayotokana na picha? | |
| 3. STADI ZA KUNUKUU<br>a) Hati za Matini Fupi. | Mwanafunzi aweze kuandika kwa usahihi hati za matini fupi kwa kuzingatia taratibu za uandishi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kwa usahihi hati za matini fupi kwa kuzingatia taratibu za uandishi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika hati za matini fupi kwa kuzingatia taratibu za uandishi. | 1. Vifaa vya kuandikia.<br>2. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika kwa usahihi hati za matini fupi kwa kuzingatia taratibu za uandishi? | 13 |
| b) Imla Fupi. | Mwanafunzi aweze kuandika imla fupi kwa wepesi na usahihi na kuzingatia taratibu za uandishi. | Kwa kutumia mbinu ya imla mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kwa wepesi na usahihi na kuzingatia taratibu za uandishi. | 1. Matini fupi katika maandishi.<br>2. Matini fupi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika imla fupi kwa wepesi na usahihi na kuzingatia taratibu za uandishi? | 14 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 4. STADI ZA UTUNGAJI<br>a) Barua Rasmi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza vipengele muhimu vya uandishi wa barua rasmi. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze vipengele muhimu vya uandishi wa barua rasmi. | 1.Chati ya vipengele vya barua rasmi.<br>2. Chati ya vipengele vya barua rasmi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza vipengele muhimu vya uandishi wa barua rasmi? | 13 |
| | (ii) Kuandika barua rasmi kwa usahihi. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika barua rasmi kwa usahihi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika barua rasmi kwa usahihi. | 1. Sampuli ya barua rasmi.<br>2. Sampuli ya barua rasmi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika barua rasmi kwa usahihi? | |
| b) Barua ya Simu. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kutaja vipengele muhimu vya uandishi wa barua ya simu. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze vipengele muhimu vya uandishi wa barua ya simu. | 1. Chati ya vipengele vya barua ya simu.<br>2. Chati ya vipengele vya barua ya simu katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vipengele muhimu vya uandishi wa barua ya simu? | 13 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuandika barua ya simu. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika barua ya simu.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika barua ya simu. | 1. Sampuli ya barua ya simu.<br>2. Sampuli ya barua ya simu katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika barua ya simu? | |
| 5. STADI ZA KUTAFSIRI<br>Kutafsiri Aya Ndefu kwa Kiingereza. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza misingi ya kutafsiri. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza misingi ya kutafsiri. | 1. Chati ya misingi ya kutafsiri.<br>2. Chati katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza misingi ya kutafsiri? | 16 |
| | (ii) Kutafsiri kwa usahihi aya ndefu ya Kiswahili kwa Kiingereza. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili maana ya jumla inayopatikana katika aya.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutafsiri aya ndefu ya Kiswahili kwa Kiingereza. | 1. Sampuli ya aya ndefu<br>2. Sampuli ya aya ndefu katika maandishi ya Braille.<br>3. Kamusi.<br>4. Kamusi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutafsiri kwa usahihi aya ndefu ya Kiswahili kwa Kiingereza? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 6. KUSIKILIZA KWA UFAHAMU<br>a) Kusikiliza Matini Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kujibu kwa usahihi maswali yanayotokana na matini fupi. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali kwa usahihi yanayotokana na matini fupi. | 1. Sampuli ya matini fupi.<br>2. Sampuli ya matini katika maandishi ya Braille.<br>3. Orodha ya maswali.<br>4. Maswali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kujibu kwa usahihi maswali yanayotokana na matini fupi? | 14 |
| | (ii) Kueleza kwa usahihi ujumbe unaopatikana katika matini fupi. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza kwa usahihi ujumbe uliomo katika matini. | 1. Matini fupi katika maandishi.<br>2. Matini fupi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza kwa usahihi ujumbe unaopatikana katika matini fupi? | |
| 7. MAWASILIANO<br>a) Kueleza Matukio. | Mwanafunzi aweze kutoa taarifa ya tukio lililotokezea kwa ufasaha na usahihi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya ripoti mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa taarifa ya tukio lililotokezea kwa ufasaha na usahihi. | 1. Chati za matukio mbali mbali.<br>2. Kanda ya video CDs./ DVD<br>3. Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza tukio lililotokezea kwa ufasaha na usahihi? | 14 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa taarifa za matukio kwa ufasaha na usahihi. | | | |
| b) Kueleza Umuhimu wa Vitu Mbali mbali. | Mwanafunzi aweze kutoa maelezo sahihi ya umuhimu wa vitu vilivyomo katika mazingira yake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza umuhimu wa vitu vilivyomo katika mazingira yao.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maelezo ya umuhimu wa vitu katika mazingira yao. | Sampuli za vitu mbali mbali. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maelezo sahihi ya umuhimu wa vitu vilivyomo katika mazingira yao? | 14 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Kongamano. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza dhana ya kongamano. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza dhana ya kongamano. | - | Je, mwanafunzi anaweza kueleza dhana ya kongamano? | 15 |
| | (ii) Kueleza jambo kwa kujiamini na ufasaha. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza jambo kwa kujiamini na ufasaha.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza jambo kwa kujiamni na ufasaha. | 1. Chati ya vipengele vya kongamano.<br>2. Chati ya vipengele vya kongamano katika maandishi ya Braille.<br>3. Kanda za video.<br>4. CDs./ DVD. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza jambo kwa kujiamini na ufasaha? | |
| 8. FASIHI SIMULIZI<br>a) Hadithi Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni hadithi fupi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubuni hadithi fupi. | 1. Chati ya vipengele vya hadithi.<br>2. Chati ya vipengele ya hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubuni hadithi fupi? | 15 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kutamba hadithi kwa ufasaha. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kutamba hadithi kwa ufasaha.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kutamba hadithi kwa ufasaha. | 1. Chati ya kanuni za utambaji wa hadithi.<br>2. Chati katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutamba hadithi kwa ufasaha? | |
| | (iii) Kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi. | 1. Sampuli ya hadithi katika maandishi.<br>2. Hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafunzo yanayopatikana katika hadithi? | |
| b) Methali. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni methali kulingana na muktadha. | Kwa kutumia mbinu mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya methali kulingana na muktadha. | 1. Sampuli za methali.<br>2. Methali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubuni methali kulingana na muktadha? | 14 |

| MADA KUU/ MADANDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali. | 1. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafunzo yaliyomo katika methali. | 1. Orodha ya methali.<br>2. Orodha ya methali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali? | |
| c) Misemo. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza dhana ya misemo. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze dhana ya misemo. | 1. Sampuli za misemo.<br>2. Sampuli za misemo katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza dhana ya misemo? | 13 |
| | (ii) Kutoa mifano ya misemo kulingana na muktadha. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa mifano ya misemo kulingana na muktadha. | 1. Sampuli ya misemo<br>2. Sampuli ya misemo katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa mifano ya misemo kulingana na muktadha? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kutoa maana inayojitokeza katika misemo mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maana inayojitokeza katika misemo mbali mbali. | 1. Maandiko yenye misemo .<br>2. Maandishi ya Braille yenye misemo. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maana inayojitokeza katika misemo mbali mbali? | |
| d) Nahau. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza dhana ya nahau. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu aeleze dhana ya nahau. | 1. Chati ya sifa za nahau.<br>2. Chati yenye sifa za nahau katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza dhana ya nahau? | 13 |
| | (ii) Kutoa mifano ya nahau. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa mifano ya nahau. | 1. Sampuli ya nahau mbali mbali.<br>2. Sampuli ya nahau mbali mbali katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa mifano ya nahau? | |
| | (iii) Kueleza maana ya nahau inayojitokeza katika mazingira yake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya nahau mbali mbali inayojitokeza katika mazingira yao.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa mifano ya nahau na kueleza maana yake. | 1. Maandiko yenye nahau.<br>2. Maandishi ya Braille yenye nahau. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya nahau inayojitokeza katika mazingira yake? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| e) Ngonjera Fupi Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubuni ngonjera fupi fupi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze wanafunzi kubuni ngonjera fupi fupi. | 1. Chati ya vipengele vya ngonjera.<br>2. Chati ya vipengele vya ngonjera katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubuni ngonjera fupi fupi? | 16 |
| | (ii) Kutamba ngonjera. | Kwa kutumia mbinu burudiko mwalimu awaongoze wanafunzi kutamba ngonjera. | Vifaa vya utambaji. | Je, mwanafunzi anaweza kutamba ngonjera? | |
| | (iii) Kueleza ujumbe unaopatikana katika ngonjera. | 1. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza ujumbe unaopatikana katika ngonjera.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana wenyewe kwa wenyewe, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza ujumbe unaopatikana katika ngonjera. | 1. Sampuli ya ngonjera.<br>2. Sampuli ya ngonjera katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza ujumbe unaopatikana katika ngonjera? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 9. FASIHI ANDISHI<br>Kubuni na Kuandika Riwaya Fupi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza dhana ya riwaya. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu aeleze dhana ya riwaya. | 1. Chati ya sifa za riwaya.<br>2. Chati ya riwaya katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza dhana ya riwaya? | 16 |
| | (ii) Kuandika riwaya fupi kwa kuzingatia kanuni za uandishi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi ,mwalimu aeleze kanuni za uandishi wa riwaya.<br>2. Kwa kutumia onesho mbinu, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika riwaya fupi kwa kuzingatia kanuni za uandishi. | 1. Chati ya kanuni za uandishi wa riwaya.<br>2. Vifaa vya kuandikia.<br>3. Mashine ya Braille.<br>4.Chati ya kanuni za uandishi wa riwaya katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuandika riwaya fupi kwa kuzingatia kanuni za uandishi? | |
